# MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 19/01/2022 KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI

## A. WALIOHUDHURIA:

1. Ndugu Clovis Mrutu -Afisa Uchaguzi (W) -Mwenyekiti
2. Ndugu Peter Luhanda -Afisa Ugavi (W) -Katibu
3. Ndugu Dafrosa Mkenda -A/Elimu Sekondari (W) -Mjumbe
4. Ndugu Alex Mang'ara -Afisa Mipango (W) -Mjumbe
5. Shaban O. Gwandu -Afisa Elimu Msingi (W) -Mjumbe
6. Ndugu Tafisa Mutalemwa -Mwanasheria (W) -Mshauri

## B. WAALIKWA:

1. Ndugu Innocent Nsojo -Afisa Ugavi -Sekretariati
2. Ndugu Frank Herman -Mhandisi Ujenzi -Mwalikwa

## BZ/KIL/1/01/2022: KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao. Aliwaomba ushirikiano wajumbe wote, alisisitiza uwazi wakati wa kujadili hoja, kikao kilifunguliwa rasmi mnamo saa 08:00 Mchana.

## BZ/KIL/2/01/2022: KUTHIBITISHA AGENDA

Mwenyekiti alimtaka Katibu kusoma agenda za kikao ili wajumbe wazipitie, baada ya wajumbe kuzipitia agenda hizo waliridhia kuwa ndizo ziwe agenda za kikao cha tarehe 19/01/2022

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha tarehe 08/12/2021
4. Ombi la kupitia Taarifa ya Mapendekezo ya kutoa Tuzo ya Zabuni ya Ujenzi wa Jengo la Dharura (EMD)
5. Ombi la kupitia Taarifa ya Mapendekezo ya kutoa Tuzo ya Zabuni ya Ujenzi wa Nyumba ya Mtumishi

| | | |
|---|---|---|
| [signature] | 31/01/2022 | [signature] |
| **Mwenyekiti** | **Tarehe** | **Katibu** |

6. Ombi la kupitia Taarifa ya Mapendekezo ya kutoa Tuzo ya Zabuni ya Kupangisha Jengo la Mgahawa

7. Ombi la kupitia Taarifa ya Mapendekezo ya kutoa Tuzo ya Zabuni ya Wakala wa Uzoaji wa Taka ngumu katika Miji ya Songe, Bokwa, Kibirashi na Kwediboma

8. Ombi la Ujenzi wa Jengo la Dharura (EMD) na Nyumba ya Mtumishi kwa kutumia njia ya Manunuzi ya Force Account

9. Mengineyo

10. Kufunga kikao

**BZ/KIL/3/01/2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA TAREHE 08/12/2021**

Katibu alisoma muhtasari wa kikao cha tarehe 08/12/2021 ili wajumbe wajiridhishe na Muhtasari huo na pia kwa madhumuni ya kufanya marekebisho Kabla haujasainiwa, Baada ya Katibu kusoma Muhtasari huo wajumbe waliridhia kuwa muhtasari huo ni sahihi kwa ajili ya kumbukumbu za Ofisi.

**BZ/KIL/4/01/2022: OMBI LA KUPITIA TAARIFA YA MAPENDEKEZO YA KUTOA TUZO YA ZABUNI YA UJENZI WA JENGO LA DHARURA (EMD). ZABUNI NAMBA LGA/127/2021/2022/W/01**

Katibu aliwasilisha taarifa ya Mapendekezo ya kutoa Tuzo katika zabuni ya ujenzi wa Jengo la Dharura (EMD) kutoka Kitengo cha Manunuzi na Ugavi.

Maelezo yalitolewa kuwa, Kitengo cha Manunuzi na Ugavi kimepokea Taarifa ya Tathimini na Mapendekezo ya Tuzo ya Zabuni ya Ujenzi wa Jengo la Dharura (EMD) katika Wilaya ya Kilindi. Zabuni Hii ilitangazwa katika Mfumo wa Manunuzi kwa Njia ya Mtandao (TANePS) na kufunguliwa Tarehe 07/01/2022 kupita mfumo huo wa manunuzi, baada ya ufunguzi Mkurugenzi aliunde Timu ya Tathimini na kuwasilisha taarifa

| | | |
|---|---|---|
| ......................... | 31/01/2022 | ......................... |
| **Mwenyekiti** | **Tarehe** | **Katibu** |

katika Kitengo cha Manunuzi baada ya kukamilisha kazi ya tathimini katika mfumo.

Taarifa ilionyesha kuwa katika zoezi la ufunguzi ni Kampuni tatu tu zilijitokeza kuomba zabuni hii na kurudisha kabrasha la zabuni kupitia mfumo wa Manunuzi kwa njia ya mtandao (TANePS). Taarifa ya ufunguzi ilikuwa kama ifuatavyo.

| Na. | Jina la mwombaji | Anuani | Gharama (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | New Builders Limited | 1754, Tanga | 650,180,000.00 |
| 2. | Works Contractors Limited | 31882, Dar Es Salaam | 615,148,160.00 |
| 3. | Scafford Investment Co. Limited | 31472, Dar Es Salaam | 426,768,972.00 |

Bajeti ya kazi hii ni Tshs. 300,000,000.00

Tathimini ya Zabuni ilipangwa katika Hatua tatu ambazo ni; Upembuzi wa Awali (Preliminary), Upembuzi wa Kina (Technical) na Upembuzi wa Mwisho (Post Qualification). Taarifa ilionesha kuwa wazabuni wote watatu wahakufaulu vigezo vya zabuni vilivyowekwa katika hatua ya Upembuzi wa Awali (Commercia Responsiveness), ambapo wazabuni wote walikuwa na makosa mbalimbali ambayo ni, Fomu ya zabuni, Cheti cha Kodi, Muda wa Uhai wa Zabuni, Cheti cha Usajili wa Kampuni (CRB), na Taarifa ya Benki. Hivyo katika hatua hii hakuna kampuni ambayo ilikidhi vigevyo na kupelekea kampuni zote kutolewa katika hatua hii (Non – Responsive).

Katika kabrasha la zabuni kipengele cha Maelekezo kwa wazabuni kilielekeza kuwa Mwajiri atatoa Tuzo ya Zabuni kwa Kampuni itakayokidhi vigezo vya Zabuni na kuwa na Gharama nafuu. Katika zabuni hii hakuna kampuni iliyokidhi vigezo hivyo hakuna kampuni iliyopendekezwa kupata Tuzo ya Zabuni na hivyo hakuna mshindi wa zabuni hii. Timu ya Tathimini ilipendekeza zabuni hii isitishwe na kutangazwa upya.

Kitengo cha Manunuzi kilipitia hatua zote za tathimini na kuona kuwa taarifa ilikuwa sahihi kwa kufuata taratibu zote za Tathimini ya zabuni na

| | | |
|---|---|---|
| ........................ | 31/01/2022 | ........................ |
| Mwenyekiti | Tarehe | Katibu |

hivyo kukubaliana na taarifa ya tathimini na kuwasilisha taarifa hii kwa Bodi ya Zabuni.

Bodi ya zabuni ilipokea taarifa na kuipitia kwa kina, na kuona kuwa hakuna kampuni iliyokidhi vigezo vya zabuni vilivyowekwa katika zabuni hii. Wajumbe wa Bodi ya Zabuni walipitisha mapendekezo ya Taarifa ya Zabuni. Bodi ilipendekeza kuwa zabuni hii ipitiwe upya kwanza kwa maana Gharama tu za waombaji nikubwa sana kuliko bajeti iliyopangwa, ikiwezekana Halmashauri iangalie namna ya kutekeleza kazi hii kwa kutumia njia ya Force Aaccount badala ya kutangazwa upya. Ombi limekubaliwa.

**BZ/KIL/5/01/2022: OMBI LA KUPITIA TAARIFA YA MAPENDEKEZO YA KUTOA TUZO YA ZABUNI YA UJENZI WA NYUMBA YA MTUMISHI. ZABUNI NAMBA LGA/127/2021/2022/W/02**

Katibu aliwasilisha taarifa ya Mapendekezo ya kutoa Tuzo katika zabuni ya ujenzi wa Nyumba ya Mtumishi kutoka Kitengo cha Manunuzi na Ugavi.

Maelezo yalitolewa kuwa, Kitengo cha Manunuzi na Ugavi kimepokea Taarifa ya Tathimini na Mapendekezo ya Tuzo ya Zabuni ya Ujenzi wa Nyumba ya Mtumishi katika Wilaya ya Kilindi. Zabuni Hii ilitangazwa katika Mfumo wa Manunuzi kwa Njia ya Mtandao (TANePS) na kufunguliwa Tarehe 07/01/2022 kupita mfumo huo wa manunuzi, baada ya ufunguzi Mkurugenzi aliunde Timu ya Tathimini na kuwasilisha taarifa katika Kitengo cha Manunuzi baada ya kukamilisha kazi ya tathimini katika mfumo.

Taarifa ilionyesha kuwa katika zoezi la ufunguzi ni Kampuni Moja tu ilijitokeza kuomba zabuni hii na kurudisha kabrasha la zabuni kupitia mfumo wa Manunuzi kwa njia ya mtandao (TANePS). Taarifa ya ufunguzi ilikuwa kama ifuatavyo.

| Na. | Jina la mwombaji | Anuani | Gharama (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | Ghana Building Contractors Limited | 1631, Dodoma | 216,605,638.00 |

Bajeti ya kazi hii ni Tshs. 90,000,000.00

Tathimini ya Zabuni ilipangwa katika Hatua tatu ambazo ni; Upembuzi wa Awali (Preliminary), Upembuzi wa Kina (Technical) na Upembuzi wa Mwisho (Post Qualification). Taarifa ilionesha kuwa mzabuni alifaulu vigezo vya zabuni vilivyowekwa katika hatua ya Upembuzi wa Awali (Commercia Responsiveness), ambapo mzabuni huyu alipita hatua hii na kuingia hatua ya Upembuzi wa Kina (Techinical).

Katika hatua ya Upembuzi wa kina mzabuni alishindwa vigezo viwili ambavyo ni, Uzoefu katika kazi zinazofanana na kazi hii ambazo mzabuni amewahi kuzifanya, na kujaza kwa usahihi fomu ya taarifa za Zabuni (Proper filled form of Qualification information). Hivyo katika hatua hii hakuna kampuni ambayo ilikidhi vigevyo na kupelekea kampuni zote kutolewa katika hatua hii (Non – Responsive).

Katika kabrasha la zabuni kipengele cha Maelekezo kwa wazabuni kilielekeza kuwa Mwajiri atatoa Tuzo ya Zabuni kwa Kampuni itakayokidhi vigezo vya Zabuni na kuwa na Gharama nafuu. Katika zabuni hii hakuna kampuni iliyokidhi vigezo hivyo hakuna kampuni iliyopendekezwa kupata Tuzo ya Zabuni na hivyo hakuna mshindi wa zabuni hii. Timu ya Tathimini ilipendekeza zabuni hii isitishwe na kutangazwa upya.

Kitengo cha Manunuzi kilipitia hatua zote za tathimini na kuona kuwa taarifa ilikuwa sahihi kwa kufuata taratibu zote za Tathimini ya zabuni na hivyo kukubaliana na taarifa ya tathimini na kuwasilisha taarifa hii kwa Bodi ya Zabuni.

Bodi ya zabuni ilipokea taarifa na kuipitia kwa kina, na kuona kuwa hakuna kampuni iliyokidhi vigezo vya zabuni vilivyowekwa katika zabuni hii. Wajumbe wa Bodi ya Zabuni walipitisha mapendekezo ya Taarifa ya Zabuni. Bodi ilipendekeza kuwa zabuni hii ipitiwe upya kwanza kwa maana Gharama tu za waombaji nikubwa sana kuliko bajeti iliyopangwa, ikiwezekana Halmashauri iangalie namna ya kutekeleza kazi hii kwa

| ............................. | 31/01/2022 | ............................. |
|---|---|---|
| **Mwenyekiti** | **Tarehe** | **Katibu** |

kutumia njia ya Force Aaccount badala ya kutangazwa upya. Ombi limekubaliwa.

**BZ/KIL/6/01/2022: OMBI LA KUPITIA TAARIFA YA MAPENDEKEZO YA KUTOA TUZO YA ZABUNI YA KUPANGISHA JENGO LA MGAHAWA**

Katibu aliwasilisha taarifa ya Mapendekezo ya kutoa Tuzo katika zabuni ya Kupangisha Jengo la Mgahawa kutoka Kitengo cha Manunuzi na Ugavi.

Maelezo yalitolewa kuwa, Kitengo cha Manunuzi na Ugavi kimepokea Taarifa ya Tathimini na Mapendekezo ya Tuzo ya Zabuni ya Kupangisha Jengo la Mgahawa katika Wilaya ya Kilindi. Zabuni Hii ilitangazwa katika Mfumo wa Manunuzi kwa Njia ya Mtandao (TANePS) na kufunguliwa Tarehe 18/11/2021 kupita mfumo huo wa manunuzi, baada ya ufunguzi Mkurugenzi aliunda Timu ya Tathimini na kuwasilisha taarifa katika Kitengo cha Manunuzi baada ya kukamilisha kazi ya tathimini katika mfumo.

Taarifa ilionyesha kuwa katika zoezi la ufunguzi ni Kampuni Moja tu ilijitokeza kuomba zabuni hii na kurudisha kabrasha la zabuni kupitia mfumo wa Manunuzi kwa njia ya mtandao (TANePS). Taarifa ya ufunguzi ilikuwa kama ifuatavyo.

| Na. | Jina la mwombaji | Anuani | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | Café Lyamisoza | 18, Songe | 1,440,000.00 |

Bajeti ya kazi hii ni Tshs. 3,600,000.00

Tathimini ya Zabuni ilipangwa katika Hatua tatu ambazo ni; Upembuzi wa Awali (Preliminary), Upembuzi wa Kina (Technical) na Upembuzi wa Mwisho (Post Qualification). Taarifa ilionesha kuwa mzabuni alifaulu vigezo vya zabuni vilivyowekwa katika hatua zote za tathimini.

Katika kabrasha la zabuni kipengele cha Maelekezo kwa wazabuni kilielekeza kuwa Mwajiri atatoa Tuzo ya Zabuni kwa Kampuni itakayokidhi vigezo vya Zabuni na kuwa na Ofa ya juu. Katika zabuni hii

| | | |
|---|---|---|
| ............................ | 31/01/2022 | ............................ |
| **Mwenyekiti** | **Tarehe** | **Katibu** |

Mzabuni M/s Café Lyamisoza alipendekezwa kupata Tuzo ya Zabuni na hivyo kuwa mshindi wa zabuni hii. Timu ya Tathimini ilipendekeza zabuni hii apewe M/s Café Lyamisoza kwa ada ya pango ya Tshs. 1,440,000.00 kwa Mwaka.

Kitengo cha Manunuzi kilipitia hatua zote za tathimini na kuona kuwa taarifa ilikuwa sahihi kwa kufuata taratibu zote za Tathimini ya zabuni na hivyo kukubaliana na taarifa ya tathimini na kuwasilisha taarifa hii kwa Bodi ya Zabuni.

Bodi ya zabuni ilipokea taarifa na kuipitia kwa kina, na kuona kuwa mzabuni aliyeomba amekidhi vigezo vya zabuni vilivyowekwa katika zabuni hii. Wajumbe wa Bodi ya Zabuni walipitisha mapendekezo ya Taarifa ya Zabuni kuwa zabuni apewe M/s Café Lyamisoza kwa kiasi cha Tshs. 1,440,000.00 kwa Mwaka. Ombi limekubaliwa.

**BZ/KIL/7/01/2022: OMBI LA KUPITIA TAARIFA YA MAPENDEKEZO YA KUTOA TUZO YA ZABUNI YA WAKALA WA UZOAJI WA TAKA NGUMU KATIKA MIJI YA SONGE, BOKWA, KIBIRASHI NA KWEDIBOMA**

Katibu aliwasilisha taarifa ya Mapendekezo ya kutoa Tuzo katika zabuni ya Wakala wa Uzoaji Taka Ngumu katika Mji wa Songe, Bokwa, Kibirashi na Kwediboma kutoka Kitengo cha Manunuzi na Ugavi.

Maelezo yalitolewa kuwa, Kitengo cha Manunuzi na Ugavi kimepokea Taarifa ya Tathimini na Mapendekezo ya Tuzo ya Zabuni ya Wakala wa Uzoaji Taka Ngumu katika Mji wa Songe, Bokwa, Kibirashi na Kwediboma katika Wilaya ya Kilindi. Zabuni Hii ilitangazwa katika Mfumo wa Manunuzi kwa Njia ya Mtandao (TANePS) na kufunguliwa Tarehe 18/11/2021 kupitia mfumo huo wa manunuzi, baada ya ufunguzi Mkurugenzi aliunda Timu ya Tathimini na kuwasilisha taarifa katika Kitengo cha Manunuzi baada ya kukamilisha kazi ya tathimini katika mfumo.

| | | |
|---|---|---|
| ...................................... | 31/01/2022 | .............................. |
| **Mwenyekiti** | **Tarehe** | **Katibu** |

Taarifa ilionyesha kuwa katika zoezi la ufunguzi ni Kampuni Mbili tu ilijitokeza kuomba zabuni hii na kurudisha kabrasha la zabuni kupitia mfumo wa Manunuzi kwa njia ya mtandao (TANePS). Taarifa ya ufunguzi ilikuwa kama ifuatavyo.

| Na. | Jina la mwombaji | Anuani | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | Kiziwanda Enterprises | 18, Songe-Kilindi | 10,000,000.00 |
| 2. | Ardor General Trading Limited | 6689, Kilindi-Tanga | 7,480,000.00 |

Bajeti ya kazi hii ni Tshs. 5,000,000.00

Tathimini ya Zabuni ilipangwa katika Hatua tatu ambazo ni; Upembuzi wa Awali (Preliminary), Upembuzi wa Kina (Technical) na Upembuzi wa Mwisho (Post Qualification). Taarifa ilionesha kuwa wazabuni wote walifaulu vigezo vya zabuni vilivyowekwa katika hatua zote za tathimini.

Katika kabrasha la zabuni kipengele cha Maelekezo kwa wazabuni kilielekeza kuwa Mwajiri atatoa Tuzo ya Zabuni kwa Kampuni itakayokidhi vigezo vya Zabuni na kuwa na Ofa ya juu. Katika zabuni hii Mzabuni M/s Kiziwanda Enterprises alipendekezwa kupata Tuzo ya Zabuni na hivyo kuwa mshindi wa zabuni hii. Timu ya Tathimini ilipendekeza zabuni hii apewe M/s Kiziwanda Enterprises kwa ada ya pango ya Tshs. 10,000,000.00 kwa Mwezi.

Kitengo cha Manunuzi kilipitia hatua zote za tathimini na kuona kuwa taarifa ilikuwa sahihi kwa kufuata taratibu zote za Tathimini ya zabuni na hivyo kukubaliana na taarifa ya tathimini na kuwasilisha taarifa hii kwa Bodi ya Zabuni.

Bodi ya zabuni ilipokea taarifa na kuipitia kwa kina, na kuona kuwa mzabuni aliyeomba amekidhi vigezo vya zabuni vilivyowekwa katika zabuni hii. Wajumbe wa Bodi ya Zabuni walipitisha mapendekezo ya Taarifa ya Zabuni kuwa zabuni apewe M/s Kiziwanda Enterprises kwa kiasi cha Tshs. 10,000,000.00 kwa Mwezi. Ombi limekubaliwa.

| | | |
|---|---|---|
| [signature] | 31/01/2022 | [signature] |
| Mwenyekiti | Tarehe | Katibu |

## BZ/KIL/8/01/2022: OMBI LA UJENZI WA JENGO LA DHARURA (EMD) NA NYUMBA YA MTUMISHI KWA KUTUMIA NJIA YA MANUNUZI YA FORCE ACCOUNT

Katibu aliwasilisha taarifa katika kikao kuwa amepokea ombi la idhini ya Ujenzi wa Jengo la Huduma ya Dharura (EMD) katika Wilaya ya Kilindi na Ujenzi wa Nyumba ya Mtumishi kwa kutumia njia ya Force Account kutoka katika Idara ya Afya.

Maelezo yalitolewa kuwa, Idara ya Afya inaomba kutekeleza mradi wa ujenzi wa Jengo la Idara ya Huduma ya Dharura (EMD) katika Wilaya ya Kilindi na Nyumba ya Mtumishi.

Halmashauri kupitia mpango wa bajeti ya mwaka 2021/2022 imepokea jumla ya Tshs. 390,000,000.00 kupitia Fedha za mpango maalum wa "Ustawi wa Taif ana Mapambano dhidi ya UVIKO - 19 ili kutekeleza ujenzi huo. Aidha maelekezo ya kupata fedha hizo za bajeti na matumizi ya fedha hizo kwa kutumia njia ya manunuzi ya Ushindani yalitolewa kupitia Barua ya Ofisi ya Rais TAMISEMI, yenye Kumb Na. AH. 161/164/01/103 Ya tarehe 25/11/2021 iliyoelekeza miradi inayotekelezwa kwa njia ya Ushindani kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 pamoja na miongozo mbalimbali.

Halmashauri ya Wilaya ya Kilindiilitangaza zabuni za miradi hii Miwili katika mfumo wa Manunuzi kwa Njia ya Mtandao (TANePS) na zabuni zikafunguliwa tarehe 07/01/2022. Baada ya ufunguzi timu ya tathimini iliundwa na kufanya tathimini ya zabuni hizo hadi mwisho. Aidha taarifa ilionyesha kuwa wakandarasi walioomba kazi hizo waliomba kwa gharama kubwa sana kuliko bajeti iliyopangwa, lakini pia hakuna mkandarasi aliyekidhi vigezo vya zabuni hivyo zabuni hizo kukosa wakandarasi wa kujenga. Bodi ya zabuni ilipitia taarifa hizo na kukamilisha michakato ya zabuni hizo kwa kukosa wakandarasi.

Idara ya Afya inaomba Bodi ya Zabuni kutoa Idhini ya kupitisha njia ya Manunuzi ya Force Account katika miradi hii ili zabuni hizi ziweze kuanza.

| | | |
|---|---|---|
| ............................ | 31/01/2022 ............................ | ............................ |
| **Mwenyekiti** | **Tarehe** | **Katibu** |

ujenzi wake kwa haraka, hii ikiwa ni baada ya Halmashauri kupokea barua kutoka Katibu Twala Mkoa wa Tanga, yenye Kumb Na. RM/B.30/24 VOL.1/58 ya tarehe 14/01/2022 iliyoelekeza miradi ambayo imekosa wakandarasi kwa zabuni kuombwa kwa gharama kubwa basi sasa inaweza kutekelezwa kwa kutumia njia ya Force Account

Wajumbe wa Bodi ya Zabuni walipokea taarifa na Kuipitisha. Ombi limekubaliwa.

**BZ/KIL/9/01/2022: MENGINEYO**

Kabla ya kufunga kikao, Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe katika kujadili mambo mengineyo ambayo yataboresha utendaji wa kazi za Bodi ya zabuni, wajumbe walisisitiza kuwa ujenzi wa miradi uanze mapema kwakuwa miradi mingi imekuwa ikichelewa kukamilika kwa wakati.

**BZ/KIL/10/01/2022: KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kutoa michango yao ya mawazo yenye tija kwa ustawi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, na kikao kilifungwa rasmi mnamo saa 09.30 Mchana.

| | | |
|---|---|---|
| .................................... | 31/01/2022 .................................... | .................................... |
| **Mwenyekiti** | **Tarehe** | **Katibu** |